

GREEN RESOURCES AS


SERA YA MAZINGIRA

Green Resources ni kampuni iongozayo katika Africa kwa shughuli za upandaji miti, uondoaji wa hewa ya kabon katika tabaka la hewa, utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na mbao na uzalishaji wa nishati asilia. Green Resources inaendesha shughuli zake nchini Tanzania, Uganda, Msumbiji, na pia imeanza katika Sudani ya kusini na Zambia.

Green Resources imedhamiria kufuata taratibu za utunzaji wa mazingira katika utekelezaji wa sera ya mazingira na programu za utunzaji wa mazingira katika kazi zote zifanyikazo katika makampuni tanzu ya Greenresources AS.

Ili kufanikisha haya, Green Resources inakusudia kufanya yafuatayo;

- Kuendesha shughuli zake pasipo kuharibu mazingira kufuatana na sheria, viwango na kanuni zote husika za mazingira.
- Kuhakikisha uwepo wa maboresho endelevu kwa kufanya marejeo ya kila mara ya malengo ya kimazingira yaliyowekwa.
- Kupunguza athari katika ardhi, hewa, na maji; pia kuhifadhi na kutunza bio-anuwai kupitia programu maalum za kimazingira katika makampuni tanzu yanayoshughulika na upandaji miti.
- Kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote pamoja na wakandarasi wanafahamu sera ya mazingira na wajibu wao katika utunzaji mazingira. Wakandarasi watahamasishwa kufanya shughuli zao kwa kufuata viwango vya mazingira vya kampuni.
- Kusimamia matumizi ya kemikali na kupunguza athari zake katika mazingira.
- Kutoa mafunzo na ujuzi unaotakiwa kwa wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa usalama na kutimiza wajibu wao katika majukumu yao yahasuyo mazingira pale inapowezezekana.
- Kuzuia uchafuzi wa mazingira pale inapowezezekana na kujiweka mfumo mzuri wa kukabiliana na majanga ya dharura.
- Kutekeleza na kufuata utaratibu mzuri wa kusimamia na kuhifadhi taka na kuhamasisha njia za kupunguza na kurudufu taka pale inapowezezekana, kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo.
- Kutekeleza kanuni za usimamizi endelevu wa misitu ikiwa ni pamoja na kupata na kutunza vyeti vya ubora vinavyotolewa na baraza la kimataifa la usimamizi wa misitu (Forest Stewardship Council-FSC) katika makampuni tanzu yake yanayojishughulisha na upandaji miti.
- Kuitangaza sera ya mazingira kwa jamii, mawakala wa serikali, pamoja na wadau wengine kwa kutoa nakala katika tovuti ya kampuni, ripoti na mbao za matangazo
- Kuhamasisha wafanyakazi kufanya kazi kwa kuboresha mazingira na kutambua athari za kimazingira zitokanazo na shughuli zao.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Mads Asprem", is written over a dotted line.

Mads Asprem
Mkurugenzi Mtendaji
Green Resources AS
31 December 2008